

KUTOKA BUNGENI

MASWALI NA MAJIBU

Na FRED ALFRED, Dodoma



# Serikali kujenga masoko ya samaki

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2023/2024, inatarajia kujenga masoko ya samaki saba na mialo mitatu kwa lengo la kuboresha miundombinu ya uvuvi nchini.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jijini hapa jana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, akijibu swali la Vicent Mbogo (Nkasi Kusini-CCM), aliyetaka kujua ni lini serikali itajenga masoko ya kuuzia samaki katika Kata za Ninde, Wampembe na Kala wilayani Nkasi.

Akijibu swali hilo, Mnyeti alisema serikali inaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo mwambao wa Ziwa Tanganyika.

"Katika mwaka 2023/2024, serikali inajenga masoko ya samaki saba na mialo mitatu; Wilaya ya Nkasi imepangiwa kujengewa mwalo wa Karungu.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imeingia mkataba na Mkarandarasi Nice Construction and General Supplies Ltd wenye thamani ya shilingi bilioni 1.6, kujenga mwalo wa Karungu," alifafanua Mnyeti.

Kwa mujibu wa Mnyeti, mwalo huo utakaojengwa utakuwa na miundombinu ya soko lenye chumba cha ubaridi, mtambo wa kuzalisha barafu na sehemu ya kuuzia samaki.

Aliwasihi wananchi wa Nkasi kutumia miundombinu hiyo pindi itakapokamilika, huku serikali ikitafuta fedha za kujenga masoko ya samaki katika kata hizo na nyingine.

"Serikali itaendelea kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini, kutokana na upatikanaji wa fedha na mahitaji ya maeneo husika," alisema.

**MBUNGE**

Kwa upande wake, Charles Kajege (Mwibala-CCM), alitaka kujua ni lini serikali itajenga malambo ya kunyweshea mifugo katika Jimbo la Mwibara.

Mnyeti akijibu swali hilo, alisema serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji kwa mifugo katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Alisema katika mwaka 2022/2023, serikali ilianza ujenzi wa bwawa la maji ya mifugo katika Kijiji cha Kihumbo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambao umefikia asilimia 95.

"Kazi inayoendelea hivi sasa ni ujenzi wa mabirika ya kunyweshea maji mifugo kabla ya bwawa kuanza kutumika. Pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali za kujenga mabwawa na kuchimba visima virefu kwa maji ya mifugo; bado mahitaji ni makubwa.

"Hivyo, nitoe wito kwa wakurugenzi wa halmashauri za wilaya kuwahamasisha wafugaji na wadau wengine kuwekeza katika miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo," aliagiza.

katika shule zetu tatu za msingi na moja ya sekond-

katika mili yetu, vinaonge- za uwezo wetu wa kufikiri

masuala ya lishe bora kwa jamii.

HABARI LEO UK 5.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**


Anwani ya Simu: "Uvuvi"
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
40487 DODOMA


14 Februari, 2024

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA VYOMBO VYA UVUVI NA UKATAJI WA LESENI ZA VYOMBO VYA UVUVI KWA MWAKA 2024

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inapenda kuwatangazia wananchi wote wanaojishughulisha na uvuvi kwamba, msimu wa kukata leseni za vyombo vya uvuvi umeanza tangu Januari 1, 2024. Kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009; Kanuni Na. 3 (1-4), Kanuni 4 (1-6) na Kanuni 13 (1) chombo chochote kinachojihusisha na shughuli za uvuvi ni lazima kiwe kimesajiliwa na kukatiwa leseni.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Kanuni 7(3) na (4), Chombo kilichopatiwa hati ya usajili na kupewa namba, inatakiwa namba hiyo iandikwe katika ubavu pande zote mbili za chombo. Kanuni ya 7 (1-5) na Jedwali la 3 inatoa mwongozo wa uandishi wa namba za usajili zinavyotakiwa kuwekwa katika chombo.

Zoezi la usajili na utoaji wa leseni za uvuvi litaisha tarehe 31 Machi, 2024, baada ya hapo wamiliki wa vyombo vya uvuvi watakaobainika kuwa hawajasajili vyombo vyao wala kukata leseni za uvuvi watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kulipa faini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi. Taratibu za usajili wa vyombo na Leseni za uvuvi zinapatikana katika tovuti ya Wizara (***https://www.mifugouvuvi.go.tz***), Ofisi za Kanda za Wizara na Halmashauri zote zenye shughuli uvuvi nchini.

Imetolewa na;

Prof. Riziki S. Shemdoe

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

ORD00016941

MWANANCHI UK 17.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Anwani ya Simu: **"Uvuvi"**
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
**40487 DODOMA**

**14 Februari, 2024**

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA VYOMBO VYA UVUVI NA UKATAJI WA LESENI ZA VYOMBO VYA UVUVI KWA MWAKA 2024

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inapenda kuwatangazia wananchi wote wanaojishughulisha na uvuvi kwamba, msimu wa kukata leseni za vyombo vya uvuvi umeanza tangu Januari 1, 2024. Kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009; Kanuni Na. 3 (1-4), Kanuni 4 (1-6) na Kanuni 13 (1) chombo chochote kinachojihusisha na shughuli za uvuvi ni lazima kiwe kimesajiliwa na kukatiwa leseni.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Kanuni 7(3) na (4), Chombo kilichopatiwa hati ya usajili na kupewa namba, inatakiwa namba hiyo iandikwe katika ubavu pande zote mbili za chombo. Kanuni ya 7 (1-5) na Jedwali la 3 inatoa mwongozo wa uandishi wa namba za usajili zinavyotakiwa kuwekwa katika chombo.

Zoezi la usajili na utoaji wa leseni za uvuvi litaisha tarehe 31 Machi, 2024, baada ya hapo wamiliki wa vyombo vya uvuvi watakaobainika kuwa hawajasajili vyombo vyao wala kukata leseni za uvuvi watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kulipa faini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi. Taratibu za usajili wa vyombo na Leseni za uvuvi zinapatikana katika tovuti ya Wizara (***https://www.mifugouvuvi.go.tz***), Ofisi za Kanda za Wizara na Halmashauri zote zenye shughuli uvuvi nchini.

Imetolewa na;

Prof. Riziki S. Shemdoe
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

eleza kuwa alifariki dunia mapema jana alipokuwa anapelekwa Hospitali ya Taifa

... Dar es Salaam (UDSM) katika Idara ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Anwani ya Simu: "Uvuvi"
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2647,
**40487 DODOMA**

**14 Februari, 2024**

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA VYOMBO VYA UVUVI NA UKATAJI WA LESENI ZA VYOMBO VYA UVUVI KWA MWAKA 2024

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inapenda kuwatangazia wananchi wote wanaojishughulisha na uvuvi kwamba, msimu wa kukata leseni za vyombo vya uvuvi umeanza tangu Januari 1, 2024. Kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009; Kanuni Na. 3 (1-4), Kanuni 4 (1-6) na Kanuni 13 (1) chombo chochote kinachojihusisha na shughuli za uvuvi ni lazima kiwe kimesajiliwa na kukatiwa leseni.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Kanuni 7(3) na (4), Chombo kilichopatiwa hati ya usajili na kupewa namba, inatakiwa namba hiyo iandikwe katika ubavu pande zote mbili za chombo. Kanuni ya 7 (1-5) na Jedwali la 3 inatoa mwongozo wa uandishi wa namba za usajili zinavyotakiwa kuwekwa katika chombo.

Zoezi la usajili na utoaji wa leseni za uvuvi litaisha tarehe 31 Machi, 2024, baada ya hapo wamiliki wa vyombo vya uvuvi watakaobainika kuwa hawajasajili vyombo vyao wala kukata leseni za uvuvi watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kulipa faini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi. Taratibu za usajili wa vyombo na Leseni za uvuvi zinapatikana katika tovuti ya Wizara **(https://www.mifugouvuvi.go.tz)**, Ofisi za Kanda za Wizara na Halmashauri zote zenye shughuli uvuvi nchini.

Imetolewa na:

**Prof. Riziki S. Shemdoe**
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**